MAMLAKA YA HALI YA HEWA
TANZANIA
# JARIDA LA HALI YA HEWA

**Na: 22. Msimu wa Kilimo 2018/19 Tathmini ya Kipindi cha Aprili 21-30, 2019 na Matazamio kwa Kipindi cha May 01-10, 2019**

**Muhtasari**


- Mvua za msimu zinazoendelea zitasaidia kuongeza unyenyevu kwenye udongo ambao utasaidia ukuaji wa mazao.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanashauriwa kufuata ushauri unaotolewa na maafisa ugani ili kuongeza uzalishaji wenye tija kutokana na mvua zinazotarajiwa.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azorena Siberia) ilidhoofika na ile iliyopo kusini, (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hiiilipelekea msukumo wa ukanda wa mvua, Inter-Tropical Convergence Zone (ITCZ) kuwepo katika maeneo mengi ya Tanzania hususan katika ukanda wa ziwa Viktoria pamoja na nyanda za juu Kaskazini Mashariki. Katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi joto la bahari lilikua juu ya wastani hivyo kuchangia katika kutokea kwa kimbunga *Kenneth*. Joto la bahari la chini kidogo ya wastani lilikuwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii iliweza kusababisha kuimarika kwa vipindi vya mvua katika maeneo kadhaa ya nchi hususan ukanda wa ziwa Viktoria pamoja na Magharibi mwa nchi yetu.

## MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2019

Kwa kipindi hiki cha siku kumi Mifumo ya hali ya hewa imepelekea mvua katika baadhi ya maeneo ya Ukanda wa ziwa victoria, nyanda za juu Kaskazini mashariki, magharibi mwa nchi ,maeneo ya kati na Pwani ya kusini. Maeneo haya yamepata mvua kati ya 26mm hadi 150mm. Maeneo mengine ya nchi hususani Pwani ya kaskazini ,kusini na baadhi ya maeneo ya nyanda za juu kusini magharibi yamepata upungufu wa mvua kwa kiasi cha chini ya 26mm kama ramani inavyoonyesha.




Kielelezo:1: Kiasi cha mvua katika kipindi cha April 21- 30, 2019.

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2019

Katika baadhi ya maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua hususani mikoa ya Mbeya,Iringa,Rukwa na Ruvuma zao la mahindi lilikua katika hali ya kukomaa. Hata hivyo maeneo mengi ya kati na kusini mwa mkoa wa Manyara yameendelea kupata mvua katika kiwango cha chini na hali hiyo imeathiri mazao. Kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hususani Pwani ya kaskazini yameendelea kupata mvua za chini ya kiwango ambapo maeneo ya nyanda za juu kaskazinmashariki,ukanda wa ziwa victoria yamepata mvua za kutosha katika dikadi hii.Hata hivyo mvua hizo hazijaleta mabadiliko katika shughuli za kilimo kwa msimu huu. Katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Tanga ,Morogoro na Pwani zao la mahindi liko katika hatua ya jani la tatu nakwa mikoa ya Shinyanga na Mwanza wakulima waliendelea na uvunaji wa mahindi ambayo yalipandwa kipindi cha mvua za vuli 2018. Pia mkoa wa Kagera uliendelea kupata mvua za msimu wa masika na mazao ya mahindi na maharage yalikua katika hali nzuri.

## HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2019

Kina cha maji katika mabwawa na mitiririko ya maji kwenye mito kwa maeneo yaliyoendelea kupata mvua kiliendelea kuongezeka kutokana na mvua zilizoendelea kunyesha.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 01-30, 2019

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda wa mvua (ITCZ) kupanda kuelekea kaskazini mwa dunia na kuwepo katika nchi yetu hususan maeneo ya ziwa Viktoria. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi. Joto la bahari la chini ya wastani linatarajiwa katika eneo la Kusini-mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola). Hali hii ya mifumo inaweza kupelekea ongezeko la mvua kwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu hususan katika ukanda wa ziwa Viktoria.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 01-10, 2019

Maeneo ya Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika baadhi ya maeneo.

Maeneo ya Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo machache hususan katika siku tano za mwanzo za dekad.

Maeneo ya Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba na Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata mvua zinazoambatana na ngurumo katika maeneo mengi hususan katika siku tano za mwisho za dekad.

Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kuwa makavu kwa ujumla na uwezekano wa mvua nyepesi katika maeneo machache.

Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kupata mvua katika maeneo machache hususan siku tano za mwanzo za Dekad.

Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kupata n

## MATARAJIO NA USHAURI KWA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MEI 01-10,2019

Hali ya mvua inayotarajiwa kwa baadhi ya maeneo ya nyanda za kusini magharibi ,Pwani ya kusini ,Ukanda wa ziwa victoria,nyanda za juu kaskazini mashariki,Pwani ya kaskazini na magharibi mwa nchi zitaongeza hali ya unyevunyevu wa udongo na kusaidia ukuzaji wa mazao. Hali ya upungufu wa mvua kwa maeneo ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) itapelekea upungufu wa unyevunyevu wa udongo. Mvua zinazoendelea kunyesha nchini zinatarajiwa kudumu kwa kipindi kifupi kutokana na kuisha kwa msimu wa mvua. Wakulima na wafugaji wafaute ushauri unaotolewa na maafisa ugani katika maeneo yao.

## HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MEI 01-10, 2019.

Kina cha maji kwenye mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika sehemu nyingi nchini. Hata hivyo, wananchi wanashauriwa kutumia maji hayo kwa uangalifu hususan maeneo ambayo yametabiliwa kuwa na upungufu wa mvua kama maeneo ya kati (Dodoma & Singida).

*Jarida limetayarishwa na:*

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania
Ghorofa ya 3 -Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

***S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz***